JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI IFAKARA
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA IFAKARA
Simu nambari: 0752218504 /0652480163 SANDUKU LA POSTA 148,
Web site: . www.ifakara.sc.tz
Barua Pepe: Ifakara.sec@gmail.com
KUMB. NA. ISS/JI/SAG/23 Tarehe 19/05/2021

JINA LA MWANAFUNZI…….
S.L.P……

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA IFAKARA WILAYA YA KILOMBERO MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021/2022

1.0 UTANGULIZI
Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Kidato cha **Tano,** Tahasusi ya…….. katika shule hii mwaka 2021.
Shule ya Sekondari ya Wasichana Ifakara ipo halmashauri ya mji Ifakara Wilayani Kilombero Mkoa wa Morogoro.
USAFIRI WA BASI , Kwa usafiri wa basi kama unatokea Morogoro shuka sehemu iitwayo **KIBAONI STAND ,** kuelekea shuleni ni umbali wa kilometa 1.5 Usafiri toka **Kibaoni** mpaka shuleni ni Tshs 1500/=tu kwa kutumia Bodaboda. **USAFIRI WA TRENI**
TAZARA ukitokea Dar es Salaam au mbeya shukia kituo cha Ifakara na hapo unaweza kutumia Bodaboda kwa Tshs 2000/= tu, aidha tunakutaarifu kue**puka kufika usiku!**.
Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 5 julai 2021.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA
2.1 SARE YA SHULE
• Mwanafunzi anatakiwa kuwa na mahitaji yafuatayo:-
• Mashati meupe mawili yenye mikono mirefu yenye nembo ya shule yasiyo bana mwili.*(yanapatikana shuleni)*
• Sketi rinda boksi kitambaa cha suti rangi ya damu ya mzee (maroon) sketi 2 za darasani na moja ya dark blue shamba dress **NDEFU MPAKA CHINI zingatia hili.**
• Rangi ya hijab (kijuba) ni nyeupe isiyokua na nakshi wala urembo wa aina yoyote kwa darasani na ya dark bluu (shamba dress) kwa waislamu inayofunika mikono.
• **Sw**eta la damu ya mzee lenye ufito mweupe chini
• T. shirt yenye kola ya kijivu (form six) yenye nembo ya shule

TANBIHI: Ili kuondoa UTOFAUTI WA RANGI NA MSHONO na matatizo yanayoweza kujitokeza kwa mzazi/mlezi kumnunulia mwanafunzi sare zisizolingana na mahitaji ya shule,hususani katika aina ya kitambaa na mshono unashauriwa kumtafuatia sare hapa shule kwa bei za kawaida.
(TANBIHI: NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI KABISA.

2:2 MAHITAJI MENGINE *(AJE NAYO)*

i. vifaa vya Hisabati (Mathematical set), Calculator kwa wanaosoma masomo ya Sayansi na Hesabu

ii. Dictionary kwa wanaosoma masomo ya sanaa (Art) na dissecting kit kwa wanaosoma biology.

iii. Daftari counter book walau 10 na vitabu vya tahasusi.

iv. Godoro size futi 2½' kukodi ni elfu kumi kwa mwaka, Blanketi, shuka 2 (mbili za light bluu), mto na Chandarua rangi nyeupe ya pembe nne.

v. Tranka (sanduku la chuma)1 kwa ajili ya usalama wa vitu vyake.na kufuri imara kwa ajili ya kufungia tranka.

vi. Vyombo vya chakula (sahani, kijiko, kikombe na bakuli vya mfupa au udongo) na siku ya kuripoti aivae)

vii. **Vifaa vya kazi za nje** vitakaguliwa siku ya kuripoti aje na jembe lenye mpini,fagio hard broom,fagio ya nje (chelewa),squeezer (drier),panga na dawa ya choo ARROW lita mbili.

viii. **Aje na gum boot** kwaajili ya shughuli anuai za kilimo na tochi ya betri.

ix. Taulo, Vitenge au Kanga doti moja atajifunga wakati wa kwenda kuoga.

x. Tracksuit rangi ya blue Jozi moja (atavaa wakati wa maandalio ya usiku)

xi. Gereni/chombo chochote chenye uwezo wa kutunza maji ya kunywa lita tano

xii. Viatu vyeusi vya kamba jozi mbili. Soksi nyeupe jozi mbili au zaidi.

xiii. Raba nyeusi ,jezi ya bluu wanafunzi wa sayansi na wale wa sanaa jezi nyeusi

xiv. Aje na bunda (rim) mbili za karataasi A4 moja kwa matumizi ya ofisi na nyingine kwa matumizi binafsi ataitunza mwenyewe tuna mazoezi mengi ya muda wa ziada.

KUMBUKA: * Simu haziruhusiwi kabisa na hakuna huduma ya kuhifadhi simu kwa yeyote shuleni.

3.0: MICHANGO

i. **ADA**

(RECURRENT ACCOUNT IFAKARA SECONDARY SCHOOL A/C Na. 21601100085 NMB IFAKARA

Kwa muhula Tshs 35,000/= au Kwa mwaka Tshs 70,000/=

ii. **MICHANGO MINGINE imefafanuliwa hapo chini weka katika akaunti hii**

(A/C Na. 21601100004) JINA LA AKAUNTI - UZALISHAJI MALI IFAKARA SEC. SCHOOL Benki NMB.

Mchango wa ukarabati wa samani 15,000/= Kwa mwaka

Tahadhari (hairudishwi) 5,000/= Kwa mwaka

Mchango wa mahafali 15,000/= Kwa mwaka

Matibabu 20,000/= Kwa mwaka

Taaluma 20,000/= Kwa mwaka

Ulinzi na upishi 30,000/= Kwa mwaka

Kitambulisho 6,000/= Mara moja

Nembo 2000/= Kwa mwaka

NB: MALIPO YOTE YAFANYIKE KATIKA AKAUNTI HUSIKA.

Hakikisha unaandika jina la mwanafunzi anayelipa malipo Ada, michango mingine , kwenye hati ya kuweka fedha (**bank pay in slip**) na umshauri karani wa fedha

aandike jina hilo pia..

ZINGATIA KUWA FEDHA TASILIMU HAZIPOKELEWI.

4

4.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi, Tekinolojia na Ufundi, yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya Rais– TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

 (a) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

 (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

 (c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).

 (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

 (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

 (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

 (g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na;

(i) Kutunza mali za shule.

MUHIMU:

1. Ni marufuku kuvaa kandambili wakati wa chakula katika Bwalo.
2. wageni wanao tambulika shuleni ni wale walioandikishwa kwenye faili la mwanafunzi na wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi mara moja kwa muhula yaani siku moja kabla ya mahafali ya kidato cha sita.
3. Likizo zote mwanafunzi atakapolazimika kwenda likizo ni sharti arudi nyumbani.

4.1: MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga.
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya Madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito/ kupata mimba
9. Kuoa au kuolewa
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Utoro
14. Kuwa na simu au kutumia simu ya mkononi shuleni.

5.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKABIDHIWA SHULENI NA MWANAFUNZI PINDI TU ANAPORIPOTI.

(i) Fomu ya kupimwa afya yake (Form for Medical Examination) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni

(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

Njoo na vifaa vifuatavyo:-

1. Result slip
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa

Ngailo S
MKUU WA SHULE.

FORM NO. 1
THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENTS' OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a medical Officer in respect of all Form Form V entrants.

Pupil's full name……
Age/Years……Sex……
Blood found (red and White)…….
Stool examination:…….
Urinalysis:……..
Venereal Diseases test:……..
T.B. test:……
Eye Test:……
Ears:……
Chest:…….
Spleen:……
Abdomen:……..
Urine for Pregnant:……

ADDITIONALL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. infection chronic or family disease etc.

……..
……..

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature:……..
Designation:……

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA IFAKARA
TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI……..
2. KABILA……...
3. TAREHE YA KUZALIWA…….MWEZI…….MWAKA…….
4. AMEZALIWA KATIKA WILAYA YA…….
MKOA WA……..
5. DINI……DHEHEBU…….....
6. JINA LA MZAZI/MLEZI……
(Ikiwa mzazi amefariki andika jina la mlezi hapa)
7. ANWANI YA MZAZI/MLEZI…….(KIJIJI)
…….. (TARAFA)
…… (WILAYA)
…….. (MKOA)
Na. ya simu…….
8. KAZI YA BABA/MLEZI…….
9. KAZI YA MAMA……....
10. Afya ya mwanafunzi (kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe: Taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha Daktari).
…….
…….
…….
11. Majina ya Ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi (matatu tu), anuani zao kamili na Namba zao za Simu.
(a) Ndugu…….. Uhusiano……..
……...……
……..
(b) Ndugu…….. Uhusiano…….
……..……
……..
(c) Ndugu…… Uhusiano……..
…….……
……

SAINI YA MWANAFUNZI ……..SAINI YA MZAZI/MLEZI…….....

FORM NO. 3

MKATABA/ AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi……. (jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii.
Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza.
Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote.
Nahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.
Saini ya mwanafunzi…….
Tarehe……
Shahidi
Jina kamili……..
Saini…….
Tarehe……

FORM NO. 4

AHADI YA MZAZI:

Mimi…… (jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi wa……..Kidato cha……. Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii. Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo. Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule
Saini ya Mzazi/Mlezi…….
Anuani kamili…….
Simu:……
Tarehe:…….